# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA KWANZA YA MUHULA WA 3, 2026
# GREDI YA 6 – KISWAHILI INSHA
# Muda: Dakika 40

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Andika insha yasiyopungua maneno 120 kwa kuanzia na sentensi ifuatayo:

**“Siku hiyo asubuhi, nilipoingia darasani, nilishangaa kuona wanafunzi wote wakiwa kimya…”**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

MAJIBU YA KISAHIHISHI

**Mada:** Insha ya kubuni
**Alama:** 20

## Jibu linalotarajiwa

Siku hiyo asubuhi, nilipoingia darasani, nilishangaa kuona wanafunzi wote wakiwa kimya. Hakuna aliyekuwa akizungumza kama ilivyokuwa kawaida. Nilikaa kwenye kiti changu na kumtazama rafiki yangu, Juma, lakini yeye hakusema lolote. Mwalimu wetu, Bi. Akinyi, aliingia darasani akiwa na tabasamu kubwa usoni.

Baada ya kusalimiana nasi, alituambia kuwa alikuwa na habari njema. Alituomba sote tusimame kwa utulivu kwa sababu mgeni muhimu alikuwa anakuja kututembelea. Muda mfupi baadaye, mkuu wa shule aliingia akiwa ameandamana na afisa wa elimu wa kaunti.

Afisa huyo alitupa pongezi kwa sababu shule yetu ilikuwa imefanya vizuri katika masomo na usafi. Alitupatia vitabu vipya vya kusomea pamoja na vifaa vya michezo. Wanafunzi wote tulifurahi sana na kumpigia makofi.

Baadaye, mwalimu wetu alitukumbusha kwamba mafanikio hayo yalitokana na bidii, nidhamu na ushirikiano. Siku hiyo nilijifunza kwamba kufanya kazi kwa bidii na kuwa na tabia njema huleta mafanikio. Niliondoka shuleni nikiwa mwenye furaha na azma ya kusoma kwa bidii zaidi.

## Swali la 5: Insha – Alama 20

**Maagizo:** Mtahiniwa aandike insha ya **maneno yasiyopungua 120**, akianza kwa sentensi aliyopewa:

*"Siku hiyo asubuhi, nilipoingia darasani, nilishangaa kuona wanafunzi wote wakiwa kimya…"*

## Mgawanyo wa Alama

| Kipengele | Alama |
|---|---|
| **Maudhui na mtiririko wa mawazo** | 8 |
| **Muundo wa insha** | 4 |
| **Matumizi ya lugha** | 4 |
| **Sarufi na tahajia** | 2 |
| **Uakifishaji na usafi** | 2 |
| **JUMLA** | **20** |

## 1. Maudhui na Mtiririko wa Mawazo – 8

- Maudhui yanahusiana vizuri na sentensi ya kuanzia – **2**
- Mawazo yameendelezwa kwa mantiki – **2**
- Kuna mwanzo, kiini na mwisho unaoeleweka – **2**
- Ubunifu na uhalisia wa matukio – **2**

## 2. Muundo wa Insha – 4

- Anaanza kwa sentensi aliyopewa – **1**
- Aya zimepangiliwa vizuri – **1**
- Matukio yanafuatana kwa mpangilio unaoeleweka – **1**
- Ana hitimisho linalofaa – **1**

## 3. Matumizi ya Lugha – 4

- Msamiati unaofaa na wenye utajiri – **2**
- Sentensi zimeundwa vizuri na kwa usahihi – **2**

## 4. Sarufi na Tahajia – 2

- Matumizi sahihi ya sarufi – **1**
- Tahajia sahihi za maneno – **1**

## 5. Uakifishaji na Usafi – 2

- Alama za uakifishaji zimetumiwa ipasavyo – **1**
- Mwandiko/uwasilishaji ni safi na unaosomeka – **1**

## Mwongozo wa Jumla wa Utoaji Alama

| Alama | Kiwango cha Utendaji |
|---|---|
| **18–20** | Bora sana; insha imekamilika, ina mawazo yaliyopangwa vizuri, lugha bora na makosa machache sana. |
| **15–17** | Nzuri; maudhui na muundo ni mzuri, ingawa kuna makosa machache ya lugha au sarufi. |
| **11–14** | Wastani; ujumbe unaeleweka lakini mawazo, lugha au muundo una udhaifu fulani. |
| **6–10** | Dhaifu; mawazo hayajaendelezwa vizuri na kuna makosa mengi ya lugha. |
| **1–5** | Dhaifu sana; insha ni fupi sana, haijaendelezwa au haizingatii mada. |
| **0** | Hakuna jibu linalostahili alama. |

**Kumbuka:** Mtahiniwa asiyefikia **maneno 120** apunguzwe kwa kuzingatia kiwango cha ukamilifu wa insha, lakini **maudhui, lugha, muundo na usahihi** viendelee kutathminiwa kulingana na majibu yake.